Tangazo la Upangaji upya wa Rockbridge ES **Nov 2017 – Feb. 2018**

Wilaya ya Shule za Kaunti ya DeKalb inatangaza mikutano mitatu ya umma ili kujadili upangaji upya katika maeneo ya Mountain and Clarkston.

Kituo kipya cha Shule ya Msingi ya Rockbridge kinapangwa kufunguliwa tarehe 3 Januari, 2018 kufuatia uhamisho wa muda mfupi wa miaka 2.5 hadi kampasi ya zamani ya Wadsworth. Mwaka kamili wa kwanza wa shule katika kituo hiki kipya utaanza Majira ya majani kupukutika ya 2018.

Kama matokeo ya nafasi iliyopatikana kwa sababu ya kituo hiki kipya na kikubwa, upangaji upya wa wahudhuriaji unapendekezwa ili kushughulikia shule zinazojaa kupita kiasi katika maeneo ya Stone Mountain na Clarkston. Pendekezo hili la upangaji upya, linaloratibiwa kuanza kutumika Majira ya majani kupukutika ya 2018 linaweza kuathiri shule za karibu katika maeneo hayo.

Shule za msingi ambazo zinaweza kuathiriwa:

- Allgood ES (katika eneo la Clarkston)
- Dunaire ES (katika eneo la Clarkston)
- Hambrick ES (katika eneo la Stone Mountain)
- Indian Creek ES (katika eneo la Clarkston)
- Jolly ES (katika eneo la Clarkston)
- Rockbridge ES (katika eneo la Stone Mountain)
- Stone Mill ES (katika eneo la Stone Mountain)
- Stone Mountain ES (katika eneo la Stone Mountain)

Shule za Katikati ambazo zinaweza kuathiriwa:

- Freedom MS (katika eneo la Clarkston)
- Stone Mountain MS (katika eneo la Stone Mountain)

Shule za Upili ambazo zinaweza kuathiriwa:

- Clarkston HS (katika eneo la Clarkston)
- Stone Mountain HS (katika eneo la Stone Mountain)

Mchakato wa upangaji upya unaendeshwa na raundi tatu za mchango maalum wa jamii. Punde raundi zote tatu za michango ya jamii zikikamilika, Mpango wa Upangaji upya Unaopendekezwa na Msimamizi huwasilishwa kwa Bodi ili kuidhinishwa mnamo Februari 2018.

Kumbuka: Maoni yote katika raunti hizo zote tatu zimezuiwa kwa kigezo cha upangaji upya kilichoorodheshwa hapa chini:

1. Mipangilio ya usalama na trafiki
2. Upangaji upya wa awali
3. Mitaa thabiti
4. Mipango maalum, k.m., mipango inayotoa mahitaji maalum kwa wanafunzi ambayo inahitaji nafasi ya ziada ya darasa
5. Ulainishaji wa shule kuu
6. Shughuli bora na za kiuchumi

Mchango wa Umma: Raundi 1 (Novemba 2, 2017, 6:30 PM katika Freedom MS)
Lengo la mkutano huu ni kutoa na kupokea maelezo kwenda/kutoka kwa jamii kama ifuatavyo:

1. Muhtasari wa mambo mengi yanayochangia pendelezo la upangaji upya
2. Orodha ya shule na maeneo ya mahudhurio ambayo yanaweza kuathiriwa
3. Mchango wa jumla na wa msingi kwenda/kutoka kwa jamii kuhusu mchakato na kigezo cha upangaji upya

Kumbuka: Hakuna mipango itakayotekelezwa ili kuzingatiwa na umma wakati wa mkutano huu wa raundi ya kwanza. Maoni yote yaliyopokewa yatachanganywa na utathmini wa wahudumu ili kuunda chaguo tatu za upangaji upya ambazo zitawasilishwa kwa mchango na maoni ya jamii katika mkutano wa pili.
Mchango wa Umma: Raundi 2 (Alhamisi, 30 Novemba 2017, 6:30 PM katika Clarkston HS)

Tangazo la Upangaji upya wa Rockbridge ES **Nov 2017 – Feb. 2018**

Lengo la mkutano huu ni kuwasilisha chaguo tatu za upangaji upya, na kutafuta mchango/maoni ya jamii kuhusu vipengele tofauti vya kila chaguo.

Kumbuka: Maoni kutoka kwa mkutano wa pili yatatumika kuunda chaguo moja linalopendekezwa na wahudumu kwa uwezekano wa upangaji upya, ambalo litawasillishwa ili kupata maoni na mchango wa umma katika raundi ya tatu.

Mchango wa Umma: Raundi 3 (Alhamisi, 11 Januari 2018, 6:30 PM katika Rockbridge ES)
Lengo la raundi hii ya tatu na ya mwisho ni kutoa chaguo moja linalopendekezwa na wahudumu kwa uwezekano wa upangaji upya, na kutafuta mchango/maoni ya jamii kuhusu chaguo hili.

Kumbuka: Chaguo moja linalowasilishwa linaweza kosa kuangazia chaguo lolote moja lililowasilishwa wakati wa raundi ya pili. Badala yake, chaguo hili litakuwa matokeo ya maoni yote yaliyochanganywa ya umma kutoka raundi ya kwanza na ya pili, na hata pia utathmini wa wahudumu. Kuwasilisha chaguo hili moja litasababisha mchango uliolengwa wa jamii kuhusu vipengele maalum vya mpango unaozingatiwa. Mpango huu haukusudiwi kuwa wa mwisho.

Mpango wa Upangaji Upya Unaopendekezwa na Msimamizi
Kufuatia maoni ya jamii kutoka kwa raundi zote za mchango wa umma (na hasa chaguo la hivi karibuni linalopendekezwa na wahudumu), Msimamizi atafanya mabadiliko yoyote yanayoonekana muhimu na kuwasilisha Mpango huo wa Upangaji upya unaopendekezwa na Msimamizi ili kuidhinishwa na Bodi.

Idhini ya Bodi (Februari 2018)
Idhini ya bodi inatarajiwa Februari 2018, na marekebisho yoyote ya eneo la mahudhurio yataanza kutumika Majira ya majani kupukutika ya 2018.

Tafadhali tembelea www.dekalbschoolsga.org/redistricting kwa maelezo na taarifa zaidi.